

MFULULIZO WA MASOMO YA AWALI KWA WALIOOKOKA.

YESU ANARUDI! TUJIANDAE.

WATU waliookoka au kuzaliwa mara ya pili hivi karibuni, wanaitwa pia Watoto wachanga kiroho. Watoto wachanga kiroho, kama walivyo Watoto wachanga wa kimwili, wanatakiwa kupwea maziwa, siyo chakula kigumu maana wanakuwa bado hawajakiweza. Biblia inasema katika **PETRO 2:2** “kama Watoto wachanga waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa (yaani yasiyochanganywa na maji), ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.”

Maziwa haya ni mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu. Mtoto mchanga kiroho anahitajika kufundishwa masomo ya mwanzo ya wokovu, halafu hatua kwa hatua atazidi kufundishwa masomo mengine mpaka yeye naye awe mwalimu wa wengine. Biblia inasema katika **WAEBRANIA 5:12-14**, “Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwamaana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya. Hatupaswi kumharakisha mtoto mchanga kiroho na kutaka kumfundisha kila kitu kwa wakati mmoja. Lazima tupambanue na kujua kipi ni chakula kigumu au mfupa asioweza kuutafuna katika uchanga wake. Tukitaka kumlisha kila kitu katika uchanga wake, tutamwua mara moja. Maandiko yanasema katika **MWANZO 33:12-14**, “Kisha Esau akamwambia, twende zetu, tusafikri, name nitakutangulia. Akajibu, Bwana wangu anajua ya kuwa Watoto ni wachanga, tena kondoo na ng’ombe nilionao wananyonyesha. Hao wanyama wataharakishwa siku moja, watakufa wote. Tafadhali Bwana wangu na apite mbele ya mtumwa wake; nami nitawaongoza polepole kwa kadiri ya mwendo wa Watoto, hata nitakapofika kwa Bwana wangu huko Seiri.”

Kila mwalimu anayewafuatilia Watoto wachanga kiroho hana budi kuwa na uchungu wa kuona Watoto hao wananyweshwa maziwa ya koroho mpaka waukulie wokovu. Hatupaswi kuzidiwa na mbwa mwitu! Mbwa mwitu, ingawa ni wanyama katili, lakini hukumbuka kuwanyonyesha Watoto wao! Biblia inaelezea juu ya jambo hili katika **MAOMBOLEZO 4:3-4** “Hata mbwa mwitu hutoa matiti, huwanyonyesha Watoto wao; bali binti ya watu wangu amekuwa mkali, mfano wa mbuni jangwani. Ulimi wa mtoto anyonyaye wagandamana na

kaakaa lake kwa kiu; Watoto wachanga waomba chakula, wala hakuna hata mmoja awamegeaye.”

Tukumbuke wakati wote kwamba haipendezi mbele za Mungu mmoja wa wadogo hawa anapopotea **MATHAYO 18:14**. Yesu Kristo aliwalinda na kuwatunza wale aliopewa, na kuhakikisha kwamba hawapotei **YOHANA 17:12**. Hatuna budi kufuata kielelezo chake (tuwalinde wale Mungu ametukabidhi kama Yesu alivyofanya). Taabu yetu itakuwa haina faida ikiwa Watoto wachanga wa kiroho tuliokabidhiwa na Mungu watakufa kiroho **WAEBRANIA 2:13, 1THESSALONIKE 3:5, 8**

Ni maombi yangu kwamba tutatumia masomo haya ya mwanzo ya wokovu kuwalinda na kuwatunza Watoto wachanga kiroho ili wasimame imara katika imeni. Tukiwaongoza wengi kutenda haki, bila shaka, tutang'ara kama nyota milele na milele **DANIEL 12:3**. Tutende kazi maadamu ni mchana, usiku waja mtu asipoweza kuanya kazi.

SOMO LA KWANZA

Furaha baada ya kutafutwa na kuonekana

Mstari wa kukumbuka **Luka 15:32** “Tena kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwakuwa huyu ndugu yake alikuwa amekufa, naye amefufuka;alikuwa amepotea naye ameonekana.”

UTANGULIZI

Wewe ndiye dada/kaka.....? Ndiyo, Nina furaha kubwa kukuona. Bwana Asifiwe sana ! Mimi ninaitwa Dada/kaka.....mimi ni mtenda kazi wa kanisa la.....

Mungu akubariki sana kwa kusikia injili ya Yesu Kristo. Ni mambo gani hasa yaliyokugusa mpaka ukakata shauri kuokoka? (hapa mpe nafasi azungumze, kama hazungumzi, mweleze kwa ufupi jinsi wewe ulivyokata shauri ukaokoka na siku yako ya kwanza ilivyokuwa baada ya kukata shauri. Mkumbushe lolote lililozungumzwa katika uumbe kwa injili katika mkutano/ibada/kushuhudia/wakati wa matendo ya ajabu nk.). Hongera. Ninakupa hongera kwa uamuzi wako huu. Ni uamuzi ambao umefurahiwa na kila mmoja aliyeko mbinguni. Uamuzi wako huu unaweza usiwafurahishe wanadamu lakini jambo moja ni dhahiri, kuna furaha kubwa mbinguni kwaajili ya uamuzi wako huu. Hata sasa malaika wanakuchungulia kwa furaha. Biblia inasema katika **LUKA 15:10** (Someni kwa pamoja mstari huu),

“Nawaambia, vivyo hivyo kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwaajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko wale tisini kenda.”

LUKA 15:7, hivyo ndivyo ilivyo, wewe sasa ni mmoja kati ya watu wachache ambao Mungu anapendezwa nao. Anakupenda sana kuliko kabla ya uamuzi wako huu.

MAWAZO YA WANADAMU KUHUSU UAMUZI WAKO WA KUOKOKA

Wanadamu wengi watakuambia umepotea. Ndivyo walivyoniambia hata mimi na hivyo haitakuwa ajabu ukikabiliana na maneno hayo maana anayefanya kazi ndani yao ni shetani anayeitwa mungu wa dunia hii ambaye ndiye aliyewapofusha fikra zao na wasijue kwamba wao ndio ambao wamepotea kwa kuacha kuiamini injili ya wokovu. Shetani huyu hafurahii kabisa uamuzi wako huu na ndiyo maana atawatumia wanadamu kukuambia umepotea ili urudi kumtumikia yeye shetani tena katika dhambi. Biblia inasema juu yako katika **2WAKORINTHO 4:3-4**, “lakini ikiwa injili yetu imesitirika (maana yake imefishwa), imesitirika kwa hao wanaopotea, ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikra zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu.

MAWAZO SAHIHI YA MUNGU JUU YA UAMUZI WAKO

1. Wewe ulikuwa umepotea, lakini sasa umeonekana/amekupata mtoto wake.

Kabla ya uamuzi huu, wewe ndiye ambaye ulikuwa umepotea. Ulikuwa mwana mpotevu na tena kondoo aliyekuwa amepotea. Yesu Kristo muda wote huu tangu uzwiwe, alikuwa anakutafuta. Wachungaji au viongozo mbalimbali wa dini hawakukuambia ukweli na walizidi kukupoteza na hata ukasahau kwamba penye pumziko ni kwa Mwokozi yesu Kristo. Yesu mwenyewe ikabidi akutafute na kukuokoa katika kundi la waliopotea. Sasa umeonekana. **YEREMIA 50:6**, “watu wangu wamekuwa kondoo waliopotea; wachungaji wao wamewapoteza; wamewapotosha milimani; wamekwenda toka mlima hata kilima, wamesahau mahali pao pa kupumzika”. **LUKA 19:10** “kwa kuwa mwana wa Adamu (Yesu Kristo) alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.”

2. Wewe ulikuwa umekufa sasa umefufuka

Mtu yeyote ambaye anaishi katika dhambi kwa kuzaliwa yaani kwa kuirithi dhambi, mtu huyu ni mfu mbele za Mungu. Mbele za wanadamu wenzie anaweza kuonekana maarufu lakini mbele za Mungu hana umaarufu wowote-amekufa! Dhambi zinamfanya mtu awe mfu mbele za Mungu. Kawaida ya ulimwengu huu katika kutenda dhambi, ni kumfuata mfalme wa uwezo wa anga yaani shetani anayetenda kazi katika watu wote wanaoasi maagizo ya Mungu katika Biblia na huku wengine wanajiita wakristo. Mimi pamoja na wewe kabla ya kuokoka, tulikuwa katika watu hao, wana wa kuazi ambao ni Watoto wanaosubiri hasira ya Mungu. Katika **WAEFESO 2:1-3**, “nanyi mlikuwa wafu kwasababu ya makosa na dhambi zenu, ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho Yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tama za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili nay a nia, tukawa kwa tabia yetu Watoto wa hasira kama na hao wengine.

3. Baada ya kukata shauri kuokolewa, umekuwa hai sasa

Ulipotubu dhambi zako pale ulipoongozwa sala ya toba ulihuishwa (kuhuishwa ni kufufuliwa, kupewa uzima au kufanywa hai) pamoja na Kristo. **WAEFESO 2:4-5**, “lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwasababu ya makosa yetu; alituhisha pamoja na Kristo: yaani mmeokolewa kwa neema.

4. Furaha baada ya kutafutwa na kuonekana

Siku ile uamuzi wako kuokoka, ni siku ya kuikumbuka mno. Mimi naikumbuka mno siku niliyokata shauri kuokoka. Ni siku ya furaha kubwa na shangwe. Lakini kama ungekuwa na macho ya kuona huko mbinguni, huko furaha na shangwe iliyopo kwaajili yako kuokoka, haifananishwi. Jina lako limeandikwa sasa katika kitabu cha uzima mbinguni na ni juu yako mwenyewe kuhakikisha linabaki katika kitabu hicho kwa kung’ang’ania wokovu, maana ni wale tu walio katika kitabu cha uzima watakoikwepa jehanamu ya moto. Ukiacha wokovu tu, jina lako linaondolewa kwenye kitabu cha uzima, na linabakia kwenye kitabu cha hukumu au mauti. **UFUNUO 20:15**. Kuacha wokovu ni kulifuta wewe mwenyewe jina lako katika kitabu cha uzima. Mimi tangu niokolewe nazidi kung’ang’ania! Ni furaha ya ajabu! Ulikuwa umekufa sasa umefufuka, ulikuwa umepotea sas umeonekana. Someni kwa pamoja mara mbili hapa: **LUKA 15:32**, “Tena, kufanya furaha na

shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa maekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.

JAMBO LA MWISHO KWENYE SOMO HILI LA KWANZA

Hakuan haja ya kujadilina na mtu yeyote au kumuuliza yeyote juu ya uamuzi wako huu kana kwamba umwulize kuwa ni mzuri au mbaya. Hata kama ni ndugu yako wa karibu namna gani, au mtu wa aina yeyote Yule, usitake ushauri kwake! Kufanya hivyo ni sawa na mtuu mzima kumwomba ushauri mtu aliyekufa. Wewe ulikuwa mfu lakini sasa wewe ni hai. Wote ambao hawajaokoka ni wafu, huwezi kuuliza swali kwa mtu mfu, hata kama ni mmeo au mkeo, kwenye mambo ya Mungu lazima uwe na msimamo wako binafsi kwasababu kila mtu atauchukua mzigo wake mwenyewe, na pia, wakati mwingine wewe kwa msimamo wako unaweza ukamponya hata huyo mfu akaokoka kwaajili ya msimamo wako, kama ukiamua kuanguka mtapotea na mtakufa wote wawili. Mimi sikuhitaji majadiliano yoyote nao juu ya roho yangu! Ningefanya hivyo, nisingedumu katika furaha hii ya wokovu, na wao wasingeliokolewa, ningekuwa nimepoteza wengi pamoja nami. Mtu ambaye yeye mwenyewe hajaokoka, hawezi kupokea uamuzi wako kwa furaha. Ni wale tu waliojaliwa neema hii ndiyo wanaofahamu kwamba katika wokovu kuna furaha ya ajabu!

MATHAYO 19:11, (Someni kwa pamoja) “lakini yeye Yesu akawambia, si wote wawezao kulipokea Neno hili, ila wale waliojaliwa.” Kumbuka kaka/dada, **WAGALATIA 6:5** imeandikwa “Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe.”

MASWALI

- 1) Je, kutokana na uamuzi wako huu wa kuokoka, kuna furaha mbele ya nani? **LUKA 15:10**
- 2) Je, shetani amefurahia uamuzi wako huu wa kuokoka?
- 3) Kabla ya uamuzi wako huu wa kuokoka, wewe ulikuwa katika hali gani, na sasa uko katika hali gani?
- 4) Ni nani aliyekutafuta ulipokuwa umepotea, akakuona, halafu akakuokoa kutoka katika hatari ya kuangamia? **LUKA 19:10**
- 5) Kabla ya kukata shauri kuokoka, ulikuwa mfu kwasababu ya nini? **WAEFESO 2:11**
- 6) Je, kuna haja yoyote ya kujadiliana na mtu yeyote au kumwuliza yeyote ambaye hajaokoka kuhusu uamuzi wako huu kwamba ni mzuri au sio

mzuri? Je, kuna haja ya kutaka ushauri kwa ndugu yeyote? **MATHAYO 19:11**

- 7) Kumwuliza mtu asiyeokoka kama umefanya uamuzi sahihi au la, ni sawa na mtu mzima kumwuliza mtu mfu/maiti, kweli si kweli?
- 8) Si wote wawezao kulipokea kwa furaha jambo hili isipokuwa wale tu waliojaliwa, ndiyo au siyo?
- 9) Kla mtu atachukua furushi lake mwenyewe hvyo hakuna haja kujadiliana na mtu yeyote kuhusu roho yangu, ndiyo au siyo?

MAELEZO MENGINE

Kama ameokoka Jumapili, wakati wa matendo ya ajabu au ibada yoyote ya kanisa kuu au katika kanisa la nyumbani au katika ushuhudiaji mweleza taratibu za ibada za kanisa kuu. Mtie moyo zaidi kuhudhuria kila Jumapili, na pia mwelezee faida za kuhudhuria darasa la Biblia kila Jumapili, na pia mwelezee faida za kuhudhuria darasa la Biblia la mafundisho ya masomo yamwanzo ya wokovu kanisa kuu, na pia ibada nyinginezo kama umeokoka kwenye mkutano wa injili unaoendelea mweleze aendeleo kuhudhuria siku zote zilizobaki za mkutano. Mwelezee jinsi ambavyo kuanzia sasa utakavyokuwa ukimletea masomo mengine na kujifunza pamoja. Panga naye jinsi ya kuhakikisha anahudhuria katika ibada hizo.

Funga kwa maombi. Mshukuru Mungu kwa kumuokoa, na mwombe Mungu ambariki kwa jinsi alivyojitoa kujikuza. Mwombe Mungu kwaajili ya mahitaji yake kazi/biashara yake, nyumba yake, ulinzi wake nk.

SOMO LA PILI

HAKIKA YA WOKOVU

Mstari wa kukumbuka **Zaburi 103:12** “Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi”.

Mungu anasamehe kama mtu ameamua kutubu na kuacha uovu.

Uhakika wa Wokovu

Moja ya mbinu kadha za shetani za kuwarudisha nyuma watu waliokata shauri kuokoka, katika uchanga wao, ni kuwafanya wawe na mashaka kwamba wameokoka. (hivi mimi nimeokoka kweli au la? Mtu anajiuliza maswali mengi ya aina hiyo). Wawe na mashaka kwambbe wamesamehewa kabisa dhambi zao. Mbinu hii itatumika pia kwako, na huenda mpaka sasa umepata

mawazo ya namna hii, “wewe kweli umeokoka au unajidanganya mwenyewe?”. Mbona hakuna badiliko lolote, uko vilevile? Mbona umekasirika leo asubuhi na watu waliookoka hawapaswi kuwa na hasira?. Mpendwa, unatakiwa kuelewa kuwa, tunapokea wokovu kwa imani siyo kwa hisia au kwa kujisikia kwamba tumeokoka. Mwili wetu utakuwa uleule, na hakuna badiliko la mwili linaloonekana, lakini katika roho kuna mabadiliko makubwa yanayokuwa yametokea. Mambo ya kiroho yanatambulika kwa jinsi ambavyo linavyosema Neno a Mungu na siyo hisia zetu. Hata kama rafiki yako angekushitua asubuhi, na kukwambie wewe hujaokoka mbona umesema lile na umefanye lile, hayo yasikutoe katika mstari na kukutia mashaka juu ya wokovu wako ulioupokea. Wakati mwingine, watu wengien wanaweza wakaanza kukushitaki kwa mambo ambayo uliyatenda kabla ya kuokoka, hata kama yalikuwa ya aibu au mabaya kiasi gani, jua ya kuwa Mungu ameshakusamehe. Angalia tu Neno la Mungu linasema nini usiyaruhusu mashaka. Mungu hafurahii mtu mwenye roho ya kusitasita. Mashaka au wasiwasi havitoki kwa Mungu, na hivyo havitakiwi kututawala na kutupotosha. Mashaka na wasiwasi vyote hutokana na adui ibilishi. Mtoto hawaliwi na kuwa mtu mzima siku moja. Vivyo hivyo na mtoto wa kiroho. Sasa basi, Neo la Mungu linasema nin juu yako baada ya kukata shauri? Pale ulipojigundua kwamba wewe ulikuwa ni mwenye dhambi kwa kuzwiliwa, na kwa kutenda na ukazijutia dhambi zako kabisa, na kuamini kwamba kufa kwa Yesu Kristo msalabani ndiyo kulikuwa upatanisho kati yako na Mungu, na ukatubu dhambi zako na kuwa tayari kuziacha kabisa, mambo kadhaa yametokea kiroho katika tendo hilo.

- 1) Dhambi zako zimesamehewa, na Mungu hazikumbuki tena. Mtu yeyote anayetubu kwa dhati dhambi zake na kuwa tayri kuziacha dhambi hizo, mtu huyo dhambi zake zimesamehewa kabisa na hazikumbukiwi tena na Mungu. Anayesamehe ni Mungu, hivyo kama wewe umeshapatana na Mungu, hata kama wanadamu watakuhukumu wakitaka ufe leo hiyo haijalishi na wanajisumbua tu, mbele za Mungu, Mungu ameshakuhesabia haki. **ZABURI 103:12** “Kama mashariki ilivyo mblai na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.” **ISAYA 43:25**, “Mimi, naam, mimi ndimi niyafutaye makosa yako kwaajili yangu mwenyewe; wala sitazikumbuka dhambi zako. **WAKOLOSAI 1:13-14, 21-22** “Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake, ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi. Na ninyi, mliokuwa hapa kwanza mmefarikishwa (mmetenganishwa), tena adui katika nia zenu kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa; katika mwili wa

nyama yake, kwa kufa kwake, ili walete ninyi mbele zake, watakatifu wasio na mawaa wala lawama.”

2) Wewe sasa una uzima wa milele

Kabla ya kutubu dhambi zako, na kuziacha kwa kumwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yako, Mwana wa Mungu aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu, wewe ulikuwa katika ghadhabu ya Mungu na uzima wa milele ulikuwa mbali nae. Wewe ulikuwa mtu wakwenda jahanam. Ulikuwa chini ya hukumu. Sasa haupo tena chini ya hukumu balu uzima wa milele ni wako. Nyumbani kwako sasa ni mbinguni aliko Mwokozi wako Yesu Kristo. Tunaona haya katika **YOHANA 3:18** “amwaminiye yeye hahukumiwi, asiyemwamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini Jina la Mwana pekee wa Mungu.” **YOHANA 3:36** “amwaminiye Mwana yuna usima wa milele;asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia. **1YOHANA 5:11-13** “Na huu ndio ushuhuda ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika mwanawe. Yeye aliye naye mwana, anao huo uzima;asiye naye mwana wa Mungu hana uzima. Nimewaandikia ninyi mambo hayo ili mjue ya kuwa mnao uzima wa milele ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu. “

3) Hutapotea kamwe ukiwa mikononi mwa Yesu

Kuanzia ulipokata shauri kuokoka, wewe sasa uko mikononi mwa Yesu Kristo nay eye nia yake na mapenzi yake kabisa ni kwamba uende mbinguni huko aliko na kufurahi pamoja naye milele na milele. Mapenzi ya Mungu baba naye ni vivyo hivyo. Kwa kuwa yeye mwenye nguvu kuliko shetan na yeyote Yule, basi atahakikisha kwamba yeyote atakayetaka kukupokonya mikononi mwake na kukupoteza ili urudi katika ghadhabu ya milele hatafanikiwa. Hivyo ndivyo ahadi yake kwako. Hata hivyo wewe pia una sehemu ya kufanya ili haya yatimie kwako. Inakubidi kufanay mambo yafuatayo.

- **Uisikie sauti ya Yesu**

Sauti ya Yesu ni neno la Mungu. Inakubidi kila utakalojifunza katika Neno la Mungu yaani Biblia ulisikie na kuliweka moyoni. Ni lazima upende kusikia Neno la Mungu. Upende pia kulisoma Neno la Mungu. Upende pia kujifunza Neno la Mungu.

- **Umfuata Yesu**

Yesu ni mtii na kondoo wake inawapasa kuwa watii pia ukisikia Neno la Mungu linasema ubadilike, basi inabidi uwe mtii na kumfuata Yesu. Jambo lile analolitaka Yesu ulifanye katika Neno lake, basi lifanye mara moja. Huko ndiko kumfuata Yesu.

Usijiongoze mwenyewe katika jambo lolote. Yafuate maongozo ya Yesu ndiye mwokozi wako, lakini pia ni Bwana wako **WARUMI 10:9**. Ni lazima ukubali awe derive wako. Hapo mwanzo ulikuwa unafanya unalolitaka, lakini sasa utakuwa unalifanya analolitaka Bwana Yesu. Wokovu si kuamua chochote cha kufanya, ni kufanya kile tu ambacho Mungu amesema ufanye, usiusililize mwili wako na ulimwengu wala usiutii, mwisho wake ni mauti.

Popote Yesu anakokupeleka katika Neno la Mungu, basin a wewe mfuata huko. Mtu anayekataa kumfuata Bwana wake huyo ni mkaidi na muasi. Wewe umeokolewa katika uasi, maana dhambi ni uasi **1YOHANA 3:4**. Hivyo hupaswi kumuasi tena Bwana wako. Ukiyafanya haya, hakuna yeyote wa kukupokonya uzima wako wa milele ulioupokea. Kuanzia sasa makao yako yapo mbinguni. **YOHANA 10:27-29**. “kondoo wangu waisikia sauti yangu;name nawajua, nao wanajifuata. Name nawapa uzima wa milele;wala hawatapotea kamwe;wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao n mkuu kuliko wote;wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu.”

Je, ukifanya dhambi hutapotea:

Dhambi ni kitu cha kukichukia kabisa. Hata hivyo mtu aliyeokoka bado anaweza akawa anafanya dhambi. Unachotakiwa kufanya unapogundua kuwa umetenda dhambi ni kutubu dhambi hiyo kwa Mungu mara moja na kuiacha. Usidanganyike kwamba kwakuwa umetenda dhambi sasa hakuna wokovu tena kwako. Hapana! Hakika yako ya wokovu iko palepale. Jambo la muhimu tu ni kwamba unapotenda dhambi, unatakiwa ujisikie vibaya, ujue umemkosea Mungu, umechafua kile alichokitakasa Mungu, na ili uwe msafi, hakikisha unatumbu haraka kwa kumaanisha, pia uache usirudie tena, kwani ukifanya hivyo utakuwa unagaragara kwenye matope yale ya zamani.

Hata hivyo, mtu aliyeokoka hawezi kufanya dhambi kwa kukusudia! Anajua hili ni dhambi halafu analifanya kwa makusudi, etu halafu atatubu!mtu wa jinsi hii bado yuko gizani kabisa, hajaokolewa. Mtu aliyeokoka anachukia dhambi na akijikuta amefanya dhambi, anahusunika na kutubu maana tumeitwa katika utakatifu. Katika hatua za mwanzo za wokovu unaweza ukajikuta unaanguka hapa na pale mara kwa mara lakini inakubidi utubu na kuacha.

Cha kufahamu pia ni kwamba, ukishaokoka tu, unakuwa na mwombezi kwa Baba, atakayekuwa anakuombea muda wote kwa Mungu Baba yetu, huyu ni Yesi Kristo Mwana wa Mungu aketiye mkono wa kuume wa Mungu Baba. **1YOHANA 2:1-12**, “Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi, tunaye mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mweney haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu, wala si kwa dhambi zetu tu, bali n akwa dhambi za ulimwengu wote. **WAEFESO 1:4-5**, “kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa nia ya Yesu Kristo, sawa sawa na Uradhi wa mapenzi yake. “hivyo fahamu bila mashaka kwamba wewe umeokoka, na uzima wa milele wako. Sema Bwana asifiwe kwa furaha ya wokovu. Neno la Mungu linasema katika **WAFILIP 1:6**, “Nami niliaminilo ndilo hili ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo yesu.”

MASWALI

Ni kipi katika haya kinakuhakikishia kwamba wewe umeokoka?

(a) Neno la Mungu,

(b) marafiki zako

(c) mawazo au hisia zako

Je, hata kama ulifanya dhambi nzito namna gani kabla ya kuokolewa, ni kweli kabisa kwamba dhambihizo zimefutwa kabisa na umesamehewa na kwamba Mungu hazikumbuki kabisa? Ndiyo au siyo?

Kulingana na Neno la Mungu, ni kweli kwamba kuanzia sasa wewe ni wa mbinguni na uzima wa milele ni wako? Ndiyo au siyo?

Je, mtu aliyeokoka anaweza akafanya dhambi, kwa kukusudia kaibaa? Ndiyo au siyo?

Je, anaweza akafanya dhambi kwa namna gani? akifanya dhambi inampasa kufanya nini mara moja? eleza ka ufupi.

Je, kutokana na somo hili ni mambo yapi mawili katika haya yaliyo sahihi kwako? (a) mimi nimeokoka na sasa ninakwenda mbinguni na ili mradi nikiisikia sauti ya Yesu na kumfuata hakuna chochote cha kuzuia uzima wangu wa milele (b) sina hakika kwamba nimeokoka kwasasa labda baadaye

(c) Niaminilo ni hili, yeye aliyeanza kazinjema moyoni mwangu, ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.

SOMO LA TATU

MFAHAMU ADUI SHETANI

Mstari **1Timotheo 5:15** kwa maana wengine wamekwisha kugeuka na kumfuata shetani”

Mtu baada ya kuokoka anaweza kugeuka na kumtuata shetani tena, hasa pale ambapo hajamfahamu shetani na fikra zake **2WAKORINTHO 2:11**. Shetani ni adui yetu **LUKE 10:19**. Ni adui wa wato wote waliookoka kama alivyo adui wa Mungu.

SHETANI AMETOKA WAPI?

Shetani hapo mwanzo hakuwa adui wa Mungu. Yeye aliumbwa na Mungu kama walivyoumbwa malaika wengine. Alifanywa kuwa malaika mkuu na akapewa utukufu mwingi na Mungu. Hatimaye alikuwa na kiburi na tama ya ukubwa kaatamani eti kumpindua Mungu aliyemuumba. Akawashawishi malaika wachache (theluthi moja) kupigana na majeshi ya Mungu na matokeo yake walishindwa vibaya na kutupwa nje ya mbingu. Hivyo akawa siyo malaika mkuu tena aliyekuwa na jina la “lucifier” ambalo maana yeke ilikuwa ni “anayetoa mwanga kama nyota ya asubuhi” bali akawa sasa anaitwa shetani. **EZEKIEL 28:13-19, UFUNUO 12:7-9, ISAYA 14:12.**

Neno shetani maana yake ni adui, mshindani, mpinzani, yeye aletaye vizuizi. Kutokana na maana ya jina shetani, sasa unaweza kufahamu kazi yake. Ni kushindana, kuleta upinzani, na kuleta vizuizi kwa watu wa Mungu au watu waliookoka katika hali ya uadui kabisa ili ikiwezekana, waiache njia ya kweli ya wokovu ya kumfikisha mtu mbinguni. Shetani anajua njia hiyo, na anapowaambia watu hakuna kuokoka au watu wanaweza kumwona Mungu bila kupitia kwa Yesu ambaye ndiye njia, kweli na uzima, anawadanganya watu kwa dhahiri maana kweli yeye anajua, anafahamu kila kitu. **MATENDO 16:16-18**. Shetani anamfahamu Yesu kuwa ni Mwana wa Mungu na ndiye wa kuhubiriwa na tena anawafahamu watu waliookoka wanaohubiri na kutetea wokovu kwamba wana nguvu kubwa na ufalme wa Mungu unawasubiri. **MARKO 3:11, MATENDO 19:13-16.**

KWANINI SHETANI ANAWALETEA

UPNINZANI WATU WALIOOKOKA?

Shetanai baada ya kuasi mbinguni, yeye na malaika zake, wamekwisha kuhukumiwa. Mahali pao ni katika moto wa milele na milele. Hawana nafasi ya kutubu tena. **MATHAYO 24:41, UFUNUO 20:10**. Kwasababu uzuri wa mbingini anaufahamu, anachokifanya, ni kuwadanganya watu ili wamfuate kuteswa pamoja naye katika ziwa la moto. Hivyo atafanya kila njia kuwadanganya kuwazuia kijanja na kushindana nao ili watu waliookoka waache wokovu au wawe na wokovu wa vuguvugu tu na hatimaye watapikwe **UFUNUO 3:15-16**. Ni kama mchezo wa mpira katika kombe la dunia, anayekwenda kufunga foli anazuiwa kwa kila namna hata kupigwa ngwala na viatu.

MBINU ANAZOTUMIA SHETANI KATIKA UPINZANI

Shetani haji wakati wote kwa mtu kwa njia ambao ataifahamu kwamba ni shetani. Namna hiyo mtu atashtuka upesi. Wakati mwingi huka kama malaika wa nuru akiwatumia hata wachungaji na watu wengine waliookoka kukutoa katika kweli ya wokovu. **2WAKORINTHO 11:14-15**. Baadaya kushindwa kuzuia wokovu wako, unapookoka, shetani kama Farao, hatati tamaa. Hujaribu yeye majeshi yake kuahidi kuwarudisha waisrael yaani watu waliookoka, ili warudi kumtumikia tena shetani au farao **KUTOKA 14:5-8**. Kama vile Farao alivyokuwa hakati tamaa akawa anawafuatia waisrael ili awarudishe waendele kuwa watumwa wake, ndivyo hivyohivyo shetani hakati tamaa, anaendelea kuwafuatia watu waliookoka ili warudi kwenye dhambi/kutokuokoka, waendele kuwa watumwa na mawindo yake.

Wakati unapookoka, shetani alishindw akabisa kushindana na nguvu za Yesu Mwokozi wetu akasalimu amri **KUTOKA 12:30:36** sasa basi atatumia mbinu kukufanya uache wokovu sasa wakati bado ukiwa mchanga katika wokovu. shetani alimtumia mfalme wa Misri Farao na Herode wakati wa Yesu, kutaka kumwua Yesu na Musa katika uchanga wao **KUTOKA 1:15-22, KUTOKA 2:1-10, MATHAYO 2:13**. Mbinu za shetani zinajumlishwa katika kukushawishi uache wokovu. Biblia inasema katika **1MAMBO YA NYAKATI 21:1** “Tena Shetani akisimama juu ya Israel akamshawishi Daudi kuwahesabu Israel,”. Kushawishi ni kubadili nia ya mtu kwa kumuumba mawazo mengine juu ya jambo kinyume na mawazo ya aliyokuwa nayo mwanzo kabla ya kushawishiwa. Shetani atatumia mbinu aina mbili katika kukushawishi:

A. Yeye mwenyewe atakushawishi uiache njia ya kweli katika akili yako utaanza kuona yanaumbika mawazo kinyume na wokovu, ulioopokea na kukufanya usipige hatua yoyote ya ziada tangu ulipookoka. Mawazo hayo yanatokana na shetani. Ukiyafuata mawazo haya, unakuwa umeyafuata mawazo yako mwenyewe na tayari utakuwa umeingia katika njia isiyo njema. Kufuata mawazo yako ni uasi mbele za Mungu **ISAYA 65:2**. Ni lazima kabisa ukatae kuafikiana na mawazo yako mwenyewe yaliyo kinyume na njia hii ya wokovu

B. Atatumia watu kukushawishi uiache kweli ya wokovu.

- a) Watu wataongozana kukushawishi kurudi dhambini. Utashangaa marafiki wa zamani wakikujia kama wamealikwa kukuletea sigara na kukuambia mwendeke unywa pombe kwa visingizio kwamba wana hela nyingi na wanahitaji watu wa kuzitumia pamoja. Hata inabidi uwe mwangalifu. Watu ambao hawajaoookoka wakikuvuta kurudi dhambini usiwasikilize na zaidi sana uepukane na ushirikiano wa karibu nao watainyonya nguvu yako ya wokovu. **MITHALI 1:10, KUMBUKUMBU 13:6-8, MITHALI 24:1, HOSEA 7:8-9**
- b) Utashangaa kwamba atafanya kila njia kuona unakosa mafundisho, ili ubaki umedumaa bila kukua katika wokovu, ili hatimaye urudi nyuma na kuiacha kweli ya wokovu. Kwasababu hiyo, utaona siku ya mafundisho, ndiyo wageni wanakutembelea nyumbani, inakubidi uende nao kwenye mafundisho la sivyo utakufa kiroho. Utaona siku za mafundisho ndipo zinazuka kila namna ya kazi zinazoonekana ni nzuri kwa kukupatia kipato, na kukushawishi kukos amafundisho. Jihadhari na hali hii. Kubali kuinangamiza nafsi yako ili uisalimishe. Ni heri ukose kipato chochote lakini uhudhurie mafundisho na hatimaye uende mbinguni. **YOHANA 12:25**. Unaweza ukakutana na watu watakaokuambia mbona siku za mafundisho zimekuwa nyingi mno na mnarudi usiku? Ujue huyo ni mpinzani. Jihadhari. Unaweza kukutana na watu wanaomsema vibaya mchungaji au askofu, na kukutoa katika imani. Jihadhari. Wajibu watu hao kama Nkodem alivyowajibu walipokuwa wanamsema vibaya mchungaji Yesu. **YOHANA 7:45-51**, utashangaa pia kwamba siku za mafundisho ndiyo magonjwa yanaanza; kichwa, tumbo, mgongo nk. Ujue huyo ni mpinzani, kemea ugonjwa huo kwa jina la Yesu

na umpige shetani halafu chukua hatua. Anza kuja kanisani. Utashangaa jinsi ambavyo shetani atakavyokukimbia. Kichwa,tumbo vyote vitanyamaza kimya dakika usiyojua.

YAKOBO 4:7, 1PETRO 5:8-9.

- c) Usimwamini na kumfuata mtu yeyote aliyeokoka ambaye haji katika mafundisho. Na ameshindwa, na ameshindwa kuishi sawa na Neno la Mungu ambaye atakuambia “huna haja ya kwenda huko, unapotea, njoo kwetu n.k”. fahamu ni mpinzani anayetaka kukutoa kwenye kweli akiwa amekuja kama malaika wa nuru, kama mtumishi wa haki ni.
- d) Utashangaa Transfer au uhamisho unajitokeza ili kukuzuia usiendeleo na mafundisho. Utashangaa safari za huko na huko mbali na mafundisho inatokea. Jihadhari. Huyu ni mpinzani. Omba bila kukoma, mpige shetani, chukua hatua, tafuta ushauri kwa kiongozi. Mambo yatakuja na kuonekana kama Baraka, kume yametumwa kutuua. Jihadhari.
- e) Utashangaa unavutwa na watu kwenda mikesha kuamkia siku ya mafundisho ili siku hiyo uwe na usingizi na kushindwa kuhdhuria mafundisho. Siyo nyimbo au pambio nyingi ambazo zitatupeleka mbinguni. Ni Neno la Mungu. Yuda alikuwa miongoni mwa mitume waliokuwa wanaimba pamoja na yesu, lakini sasa yuko jehanam. **MARKO 14:17, 26**, jihadhari na mpinzani atakapokuja kwa njia hii.

SOMO LA NNE

YEYE ASHINDAYE

Ufunuo 2:7, “yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.”

Safari ya Mbinguni ni safari ya mashindano

Unapokuwa umekata shauri kuokoka, basi inabidi ufahamu kwamba umeingia katika mashindano. Yeye atakayeshinda atapata taji ya ajabu milelel. Kila siku katika wokovu itakuwa ni siku ya vita na mashindano lakini lazima tushindane na kuumaliza mwendo na kuilinda imani. **2TIMOTHEO 4:7-8**, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda;baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana mhukumu mwenye haki

atanipa siku ile;wala si mimi tu bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.” Ni lazima kuvipiga vita vya imani maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, **WAEBRANIA 11:6**, “lakini pasipo imani, haiwezekani kumpendeza;kwamaana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwambahuwapa thawabu wale wamtafutao.”. maisha ya wokovu, nimaisha ya imani;kumtegemea Mungu katika kila jambo katika maombi na Neno lake. Yeye aliyeanza kazi ndani yako ni lazima ataitimiza. Unachotakiwa, katika masindani haya ni kujizuia yote ambayo unaona yanakuja kuharibu bidii yako katika kumtafuta Mungu. Biblia inasema katika **1WAKORINTHO 9:25**, “na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo;bali sisi tupokee taji isiyoharibika.

Utashangaa kwamba wakati utakapokuwa unajitayarisha kwaajili ya kwenda kanisani kufundishwa, ndipo watakapotokea wageni nyumbani! Wage, waambie mwende wote kanisani au wakusubiri. Kwa nini waje tu wakati uko tayari kwenda kanisani? Ujue hayo ni mashindano. Piga vita vilivyo vizuri. Ilinde imani. Utashangaa siku za ibada ndipo kinatokea kila aina ya kizuizi mara hiki hakipo mara kile. Usidhani ni mambo ya kawaida, ujue ni vita, ni mashindano. Shetani hapendi uende kubarikiwa kwa kujifunza zaidi huko kanisani. Siku za kanisani usikose ziweke katika ratiba yako na shindana wakti mwingien, muda tu kidogo kabla ya saa za ibada, utaanzakuona kichwa kinaanza kuuma au tumbo! Ujue hayonimashindano. Mwombe Mungu halafu njoo hivyohivyo kwa imani. Shindana, ghafla utashangaa ugunjwa haupo tena. Kumbe yalikuwa ni mashindano tu. Uwe radhi hata kwenda kanisani kwa miguu kama hakuna nauli. Utashangaa Baraka za Mungu zitakazomiminika kwako.

Siku zote kuanzia sasa, lenga kukua zaidi katika wokovu, hivyo usikose vipindi vya mafundisho kanisani. Kila unapopata nafasi soma Biblia na fanay maombi japo mafupi kwa Bwana Yesu akusaidie kudumu katika wokovu. Shindana **1TIMOTHEO 6:12**

“piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi. “Tumia bidiii uliyo nayo, usiwe mlegevu katika kujifunza, uwe na bidii yote. Nunua daftari la kuandika mafundisho na yapitie mafundisho yote na kuyatenda. Uliza lolote usilolielewa kwa viongozi. **WARUMI 12:11** “Kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana. “lolote utakalojifunza, lisiishie katika daftari, lifanye kwa vitendo, usiwe msikiaji tu.

YAKOBO 1:22-24 “lakini iweni watendaji wa Nano, wala si wasikiaji tu. Mkijidanganya nafsi zenu. Kwasababu mtu akiwa ni msikiaji wa Neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana jujiangalia, kasha huenda zake mara akasahau jinsi alivyo.” Siku hadi siku zidi kustahimili katika yote. Tukistahimili tutamiliki pamoja naye. **2TIMOTHEO 2:12.** “kama tukistahimili tutamiliki pamoja naye; kama tukimkana yeye, yeye naye atatukana sisi”.

Usikubali kamwe kurudi nyuma katika wokovu ulioupokea. Usimkane Yesu halafu, naye aje akukane. Shindana hadi mwisho. Yako mengi mno ambayo utazidi kujifunza kila siku kanisani yashike na yatendee kazi. Siku chache zijazo na wewe utakuwa mwalimu wa ufuatiliaji ukiwafundisha wengine waliookoka nyuma yako ili nao wasimame katika wokovu kiume. Ni lazima ushinde katika Jina la Yesu. Karibu zaidi kanisani kwa mafundisho mengine. Kumbuka mstari ufuatao: **UFUNUO 2:7** “Yeye aliye na sikio na alisikie Neno hili ambalo roho ayaambia makanisa. Yeye alshindaye, nitampa matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.

SOMO LA TANO

KUJARIBIWA KWA IMANI YA MTU ALIYEOKOKA

Mstari wa kukumbuka. **1PETRO 1:6-7**, “Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo ikiwa ni lazima mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali, ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuw ahiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekana kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo.

KUJARIBIWA KWA IMANI

Imani ya mtu aliyeokoka ni ya thamani kuu kuliko dhahabu. Ili kuijaribu dhahabu na kuithibitisha kwama ni dhahabu safi, hutumika moto. Dhahabu safi inapopitishwa katika moto mkali, kutoka ikiwa imeng’aa zaidi. Vivyohivyo, ili kuijaribu imani ya mtu aliyeokoka, na kuithibitisha kwamba ni imani safi, imani hiyo hujaribiwa kwa kupitishwa katika maudhi na mateso. Mtu anayestahimili na kushinda, kwa kuvumilia maudhi na mateso yoyote yanayoletwa kwake kwa ajili ya imani yake ya wokovu; ndiye ambaye atakayeonekana ni mwenye sifa na utukufu na heshima wakati wa kuja kwake Yesu Kristo. Maudhi haya na mateso ni kawaida kwa kial matu aliyezaliwa kwa

roho au kuzaliwa mara ya pili au kuokoka; na hayapaswi kufikiriwa kuwa ni kitu kigeni. **1PETRO 4:12**

Waliozaliwa kwa mwili huwaudhi waliozaliwa kwa roho. Tangu zamani hata sasa, watu waliozaliwa kwa mwili yaani watu ambao hawajaokoka, au wale wanaofuata dini tu, huwaudhi, huwatesa na kuwanenea mabaya watu waliozaliwa kwa roho yaani watu waliookoka. Hivyo, siyo kitu kigeni mambo haya yakimpata mtu aliyeokoka nyakati hizi. Tunasoma katika **WAGALATIA4:29** “lakini kama vile siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili alivyomuudhi Yule aliyezaliwa kwa roho, ndivyo ilivyo na sasa. “

Yesu Kristo alichukiwa, aliudhiwa, alinenewa mabaya tena aliteswa kiongozi mkuu wa wokovu wetu Yesu Kristo, alikamilishwa kwa njia ya mateso. **WAEBRANIA 2:10**. Yesu aliudhiwa **YOHANA 5:16**, walimwita ana pepo **YOHANA 8:48, YOHANA 7:17**. Ulimwengu, yaani watu ambao hawajaokoka walimchukiana kutafuta kila njia ya kumuua. **YOHANA 7:19, YOHANA 8:37, YOHANA7:20**. Yesu alikukiwa bure, yaani bilsa sababu yoyote. **YOHANA 15:24-25**. Walimwita amerukwa na akili **MARKO 3:21**

Vivyo hivyo kwa nyakati zetu. Mtu aliyeokoka atachukiwa, ataudhiwa na kuteswa na watu wasiookoka, na kupew akila majina ya dhihaka. Yesu Kristo alitujulisha mambo haya mapema kama tunavyosoma katika **YOHANA 15:18-21** “iwapo ulimwengu ukiwachukia mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukuaninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake;lakini kwakuwa ninyi si wa ulimwengu.....

Pia soma pale Yesu aliposema ya kuwa...kama mti mbichi umetendewa hivi, itakuwaje kwa mti mkavu? Pale alipokuwa amebeba msalaba halafu wanawake wa Israel wakawa wanamlilia.

Bali mimi naliwachagua katika ulimwengu kwasababu hiyo, ulimwengu huwachukia. Likumbukeni lile Neno nililowaambia, mtuwa si mkubwa kuliko Bwana wake, ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi. Ikwa walishika Neno langu watalishika na lenu. Lakini haya yote watatenda kwa ajili ya Jina langu, kwakuw ahawamjui yeye aliyenipeleka.

WATAKATIFU WOTE WALIUDHIWA

KUSHITAKIWA NA KUTESWA

Tangu zamani, watu wa Mungu walipitia maudhi na mateso. Yusufu aliudhiwa na kutendwa machungu hata na ndugu zake. **MWANZO 49:22-23**. Musa alishutumiwa na kuteswa **WAEBRANIA 11:24-25**. Watakatifu wengi waliumizwa vibaya hata kupigwa kwa mawe na kukatwa kwa misumeno **WAEBRANIA 11:32-38**. Pia kumbuka namna kina Paulo walivyopigwa mijeledi na kuvuliwa nguo mbele za watu.

Ayubu aliyekuwa mwenye haki na mtimilifu, alichekwa sana na majirani zake na kufanywa kicheko. Hata mkewe alimgeuka. **AYUBU 12:4**. Ayubu alikuwa machukizo kwa ndugu zake, rafiki zake, na wake na watu wasio haki. Hata Watoto walimdharau na kumdhihaki. **AYUBU 19:13-19, 30:9-10**. Watakatifu katika kanisa la kwanza walifanywa takataka za duinia. **1WAKORINTHO 4:10-11**. Hata hivyo, walijipatia sifa njema katika hayo, kwa kuvumilia kila aina ya mateso na maudhi na kuendelea katika imani. **2WAKORINTHO 6:4-10**. Mtume Paulo alipitia kila namna ya mateso kwa ajili ya imani yake **2WAKORINTHO 11:23-27**.

WAFUASI WA BWANA YESU NI WALE

Wanaoendelea kushika Neno katika dhiki nyingi. Mtu aliyeokoka ambaye ataamua kuacha wokovu kutokana na kukwepa dhiki au udhia, Yesu anamwita mtu aliyepandwa mbegu peny amiamba na hamfurahishi Mungu kabisa. **MATHAYO 13:20-21**. Wafuasi halisi wa Bwana Yesu, ni wale ambao wataendelea katika wokovu pamoja na dhiki watakazokutana nazo. Angalia andiko lile, mtu aliyeamua kulima, akiwa anageukageuka nyumba, huyo sio mwanafunzi wake Yesu. Pia, mtu akitaka kumfuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalama wake(awe tayari kwa lolote) na amfuate Yesu. Wafuasi halisi ni wale wanaovumilia na kuendelea. **1WATHESALONIKE 1:6**. Imetupasa kuingia mbinguni kwa njia ya dhiki nyingi. **MATENDO 14:21-22**.

MAUDHI TOKA KWA WAZAZI, MUME AU NDUGU

Kama tulivyoona kwake Yesu na watakatifu waliotutangulia, sisi sote hatuna budi kuudhiwa kwaajili ya imani ya wokovu. Ni kawaida kabisa mwanamke aliyeolewa kuudhiwa na mumewe ambaye hajaokoka. Ni kawaida kuudhiwa na wazazi au ndugu ambao hawajaokoka. Utaitwa umechanganyikiwa, au umerukwa na akili n.k kama walivyofanya kwa Yesu tu.

Na majina haya ni ya kawaida kutoka kwa watu wasiokuwana imani ya wokovu. Ikiwa tunaitwa tumerukwa na akili zetu, ni kwaajili ya Mungu na hata watu waliookoka katika kanisa la Kwanza walipewa majina hayo. **2WAKORINTHO 5:13**. Mumeo anaweza kukupiga makofi na fimbo kwa ajili ya wokovu na kukusingizia kwa wengi ili uache wokovu. Haya ya sikufanye uache wokovu. Ukipigwa makofu kwaajili ya wokovu, ndo ndo wema haswa mbele za Mungu. **1PETRO 2:19-21**. Unaweza ukapigwa pia na wazazi au ndugu, vumilia tu. Unaweza ukanyimwa fedha za chakula na mumeo, fedha za matumizi kutoka kwa wazazi au ndugu na kutishiwa kunyimwa kila kitu, endelea tu na wokovu. Itatufaidia nini tukiupta ulimwengu wote na kupata hasara ya nafsi zetu, tutakapotupwa katika ziwa la moto, tukapata hasara ya nafsi zetu, tutakapotupwa katika ziwa la moto? **MARKO 8:36**. Wazazi na ndugu wanaweza kukuweka katika kikao na kukwambia; hivi umewahi kusikia kwamba kunamtu aliyeokoka katika ukoo wetu? Mbona unakuwa wa kwanza kuvuruga ukoo wetu?

Maneno yote haya hayatoki kwa Mungu, ni shetani anawatumia, wala haina haja ya kuwachukia. Yesu Kristo alikuwa ndiye wa kwanza kutumika kwa Mungu katika familia yake, na yeye pekee ndo alikuwa wa kipekee kulinganisha na wenzie. Nduguze waliuwa bado hawajaamua kumfuata. **YOHANA 7:2-5**. Baadaye nduguze walikuja nao kufunuliwa kuhusu wokovu, mingoni mwao akiwa Yakobo aliyekuwa Mtume **WAGALATIA 1:19**. Mungu amekupa neema wewe kuwa wa kwanza, wengine nao watafuata. (je ni wangapi wameokoka kwenu?). mbona hawasemi kwnaini unataka kwenda chuo kikuu, mbona hujamwona yeyote aliyepata digree katika ukoo wetu? Jipe moyo, ulimwenguni tunayo dhiki, lakini tujipe moyo, Yesu alivyoshinda, sisi nasi tutashinda. **YOHANA 16:33**

Watatuita tumepotea.

Baada ya kuokoka, inatulazimu kuyaacha mafundisho manyonge tuliyokuwa tunayatumikia katika madhehebu yasiyohubiri wokovu. **WAGALATIA 4:9**. Hatuwezi kuendelea na sanamu au divai inayolevya nk. Kwa jinsi hii, mara nyingi imetulazimu kuacha madhehebu yetu ya kwanza na kujiunga na madhehebu yanayofundisha wokovu na kulisimamisha Neno la Mungu katika mambo yote. **WAGALATIA 1:14-16**. Tunapofanya hivyo, tunafanya kama alivyofanya Petro, Yohana, Paulo na wengineo na huku siyo kutangatanga, Yesu Kristo alitushauri tufanye hivyo kwa kutufundisha kwamba yatupasatuwe kama mfanya biashara anayetafuta lulu nzuri. Akiiona, huuza alivyo navyo akainunua **MATHAYO 13:45-46**. Sisi nasi tutaliacha dhehebu

ambalo silo “lulu nzuri” ya kutuwezesha kujifunza Neno la Mungu na kuw amsaada kwetu kufika mbinguni. Sasa basi, tutapofanya hivi, mara kwa mara tunaitwa, “tumepotea”. Jina hili tunaweza tukapewa na watu wasiiokoka au hata waliookoka ambao wameshindwa kuviacha vyote navyo na kumfuata Yesu, au hata wale ambao wamemezwa na udhehebu. Wameshindwa kuacha madhehebu yao kwa kupenda utukufu wa wanadamu **YOHANA 12:42-43, LUKA 14:33**. Ili tuweza kushinda katika jaribu hili la imani yetu, inatupasatufahamu kweli ya Neno la Mungu inayoeleza ni akina nani hasa ambao wamepotea. Tukilifahamu kweli, hiyo kweli, hiyo kweli itatuweka huru, na kufahamu bila mashaka kwamba hatujapotea bali tumetoka upotevuni na kuingia katika njia halisi ya uzima. Kwao hao wanaotuita tumepotea ni ishara ya kipotea, bali kwetu ni ishara ya wokovu **WAFILIP 1:27-28**

TAFSIRI 11 ZA KIBIBLIA ZA MAANA YA WATU WALIOPOTEA

- (a) Watu wanaositasita katika mawazo mawili-kumtumikia Bwana Yesu n akumtumikia shetani, ulimwengu. **WAEBRANIA 10:37-39, 1WAFALME 18:21**
- (b) Watu wasiozijua njua za Mungu na hivyo kufuata mapkeo ya wanadamu katika kufanya mambo. **ZABURI 119-210**
- (c) Watu wasioyajua maandiko, hivyo kuyapotosha na kuyatafsiri visivyo **MATHAYO 22:29**
- (d) Watu waliokwenda mbali na kweli na Neno la Mungu **YAKOBO 5:19**
- (e) Watu wanaotetea divai au kileo cochote na kudai kwamba Mungu amekihalalisha wakati mbele za Mungu kileo chochote ni matapiko na uchafu **ISAYA 28:81**
- (f) Watu wanaoacha kulisikia na kulifuata Neno la Mungu linalofundishwa na watumishi wa mUngu wanaofundisha au kuisimamia kweli yote ya Neno la Mungu **1YOHANA 4:6**
- (g) Watu ambao injiili ya wokovu imefichwa au kusitirika kwao na shetani ambaye ndiye Mungu wa dunia hii, anafanya kazi ndani ya maisha yao; wakimtumikia na huku wakisema hakuna kuokoka. **2WAKORINTHO 4:3-4**

- (h)** Watu wasiopata maonyo yaliyo katika Neno la Mungu. Bali wamefanywa wajinga kwa kufarijiwa kwamba wanwkwenda mbinguni, huku maisha yao yakiwa hayaendi sawa na Neno la Mungu **MITHALI 5:23**
- (i)** Watu wanaoiacha njia iliyonyooka yaani Neno la Mungu, na kufuata njia za wenyewe katika kusema, kuwaza na kutenda. **2PETRO 2:15**
- (j)** Watu wanaofuata vinyago vyao (dhehebu Fulani, mchungaji Fulani, Askofu Fulani, mwinjilist fulani)Badala ya Neno la Mungu. **EZEKIEL 44:10**

WAJIBU WETU wakati tunapoudhiwa au kudhihakiwa na kuteswa kwaajiili ya wokovu

- a)** Inatupasa kuendelea na wokovu na kuwaacha waseme huku sisi tukikaa kimyaa, usijibizane nao. **AYUBU 21:3**
- b)** Hatupaswi kurudisha matukano wala kuwalipoza kisasi bali tukijikabidhi tu kwa Mungu katika maombi tunapofikiwa na hayo. **2PETRO 2:23, WARUMI 12:18-19**. Inatupasa kuushinda ubaya kwa wema **WARUMI 12:20-21**
- c)** Inatupasa kuwapenda tu na kuwaombea wanaotuudhi na kututesa **MATHAYO 5:44-45**
- d)** Haitupasi kuwaogopa wauuao mwili, kisha wasiweze kuua na roho, inatupasa kumwogopa Mungu awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika ziwa la moto. **MATHAYO 10:28, 1PETRO 3:14**
- e)** Haitupasi kujaribu kutafuta amani kwa kuacha wokovu na kufuata masharti yao. Huku ni kumkana Yesu **MATHAYO 10:39**. Wakituona tumesismama imara katika imani yetu bila kutetemeka na maudhi yao, mwishoni hawataendelea kufanay wanayotufanyia na tutawavuta katika wokovu.
- f)** Hatupaswi kuwatii wazazi au mume wanapotuelekeza kufanya yaliyo kihyume na Neno la Mungu kama kuacha kusali au kuacha wokovu. Tuwatii katika Bwana tu. Yaani tuyatii yale ambayo ni sawa na maagizo ya Mungu. **WAEFESO 6:1**. Mke anapaswa kimtii sawasawa na maagizo yaele tu ambayo Kristo anayolipa kanisa lake **WAEFESO 5:24**. Kristo hawezi kuliambia kanisa lake kuacha kusali nk.

Inatupasa kuamini kwamba Mungu hatimaye atatuepusha na maudhi hayo. Kwa kila jaribu kuna mlango wa kutokea. Mateso ya mwenye haki ni mengi lakini Bwana humponya nayo yote. Inatupasa kudumu katika maombi bila kukoma. **1WAKORINTHO 10:13, ZABURI 34:19, 1PETRO 5:10-11, WATHESALONIKE 5:17-18**

Dhehebu linalolimamia kweli ya Neno la mungu hunenwa vibaya kila mahali. Vivyo hivyo hata kwa watu waliosimama vizuri mbele za Mungu.

Hatupaswi kubabaika tunapooni pale tunapohamia pananenwa vibaya kila hamali na kuzushiwa kila namna ya uongo. Hii ni kawaida. Kanisa la kwanza, lininenwa vibay akila mahali. **MATENDO28:22**. Pia ujue, silaha kubwa anayotumia shetani kupambana na watu wa Mungu, ni silaha ya uzushi, anazusha jambo, hadi watu waje waamini kuwa ilikuwa si kweli, muda mrefu umepita, na yeye ameshafanya maangamizi kwa watu aliokuwa anawazuia kuingia kwenye kanisa hili, au vyovyote vile kwa watu.

AINA NYINGINE YA KUJARIBIWA NA IMANI

Wakati mwingine baada ya kuokoka, kutokana na msimamo wako wa imani, unaweza ukakuta biashara yako haiendi vizuri kama mwanzo, fedha zikapungua kiasi cha kukosa mahitaji yako ya kila siku, ukafukuzwa kazi, ukaibiwa vitu na fedha au kuandamwa na hali ambazo ni nzito. Hi ni kawaida. Mkuu wa ulimwengu huu sh etani, hufanya kila namna kututikisa ili tuache imani. Yote haya ni kujaribiwa kwa imani yetu. Ni mtihani wa imani. Tunaposhikilia na kushinda Mungu hufurahishwa sana nasi.

Thawabu kubwa kwa wote washindao baada ya kujaribiwa kwa imani yao.

Kuna thawabu kubwa kwa kila mtu ambaye ataendelea na wokovu pamoja na kujaribiwa kwa imani yake. Huko ndiko kweli kumpenda yesu. Aupendaye katika dhiki ndiye rafiki. **MATHAYO 5:10-12, 1PETRO 4:12-14**. Jambo la kuangalia tu ni kwamba, haitupasi kuudhiwa na kuteswa kwa sababu ya kufanya dhambi. Huko si kujaribiwa kwa imani. **1PETRO 4:15-16**

Mwisho, tafakari mistari ifuatayo:- **ZABURI 129:2, ZABURI 69:7-8,13, ZABURI 37-38, ZABURI 37:32-33, ZABURI 27:10, ZABURI 27:1-4. MITHALI 29:27, MATHAYO 10:22**

SOMO LA SITA

SIO KUMWAMINI TU ILA KUTESWA KWA AJILI YA KRISTO

Mstari wa moyo:- **Wafilipi 1:29** “maana mmepeewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila n akuteswa kwaajili yake”.

Baada ya kumwamini Yesu Kristo, na kuanza kukiri wokovu uliopokea hadharani, kutafuata kila namna ya kebehi. Kutukanwa na kila namna ya kuchukiwa na ndugu zetu wa karibu. Yesu aliacha ametuambia kwamba inabidi tuvumilie hayo yote mpaka mwisho. Tunasoma katika **MATHAYO 10:22**, “nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu kwaajili ya Jina langu; lakini mwenye kuvumilia hata mwisho ndiye atakaye okoka”. Baada ya kuokoka na kuanza kuukiri wokovu hadharani, na kuanza kufahamika huku na huko kwamba umeookolewa, wazazi, ndugu, mme, mke marafiki na wengineo wataanza kuwa kinyume nawe. Kinyume cha matarajio yako. Katika hali ya kawaida, ungefikiria, wazazi, mume au mke wangekufurahia kwa kuokoka kwako, lakini haitakuwa hivyo kabisa. Wengine watasema umeachadini ya ukoo wako wote na kupotea ukabadili dini. Je!uliomba ushairu kwa ndugu zako na wazazi wako?

Yote haya watakuuliza kwasababu hawajui ile kweli ya injili, au wameshika mapokeo ya zee tu! Hali hii itavuruga sana uhusiano wako na mumeo, mkeo, ndugu zako na wazazi. Amani kwa kiasi Fulani itavurugika katika jaaa zako. Kutakuwa na msugvano! Usihangaike, haya hayana budi kutupata maana Yesu Kristo hakuja kuleta amani bali mafarakano. **LUKA 12:51-53** “Je, mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia, la sivyo, bali mafarakano. Kwa kuwa tokea sasa katika nyumba moja watakuwamo watano wamefarakana, watatu kwa wawili;wawili kwa watatu. Watafarakana baba na mwanawe na mwana na babaye;mama na binti yake, na binti na mamaye;mkwe mtu na mkwewe, mkewe n amkwewe mtu etc.

Unaona wokovu utaleta mafarakano! Utashanga akwamba utafaniwa hata na vikao na kuteswa. Kumbuka umepewa si kumwamini Yesu tu, ila na kuteswa kwaajili yake. Utapewa majina ya kila namna. Utaitwa umechanganyikiwa, akili zimekuruka, na kila namna ya majina.

Kumbuka haya alifanyiwa Bwana Yesu Kristo. Aliitwa mkuu wa pepo. Sembuse sisi aliotuuma? Imeandikwa katika **MATHAYO 10:24-28**, manafunzi hampiti mwalimu wake wala mtumwa hampiti bwan wake. Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake,na mtumwa kuwa kama bwana wake. Ikiwa wamemwita mwenye nyumba (Yesu) Beelzebul (mkuu wa pepo) je! Si zaidi ya wake walio wa nyubani mwake? (wale waliookoka kwa Neno lake). “msiwaogope

wao wauuuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni Yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanamu.

Baada ya kulikulia Neno la Mungu, hayo yatatupata. Lakini ni kwasababu sisi siyo wa ulimwengu huu tena, ndio maana watu wa ulimwengu huu watachukia; “kwa kuwa wao si wa ulimwengu kama mimi nisivyo wa ulimwengu” chuki hiyo inaweza ikasababisha kuteswa, kunymwa chakula, kunyimbwa fedha za matumizi, ada, kupigwa amakofi na kuteswa ili uache wokovu. Vumilia, shik asana ulichonacho asije mtu akaitwaa taji yako. Biblia inasema **UFUNUO 3:11**, “Naja upesi, shika sana ulichonacho, asije mtu akaitwaa taji yako.”

Watu wanaokwenda mbinguni, ni lazima wapiti katika adha, mateso, dhiki, ni lazima waudhiwe kwaajili ya haki. **MATENDO 14:22**. Imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi. Erw

MATHAYO 5:10 “Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki, maana ufalme wa mbinguni ni wao. Yeyote aliyechagua njia ya okovu au maisha ya utaua, yaani utakatifu lazima utaudhiwa ili ukatishwe tamaa.

Jipe moyo utashinda. **1TIMOTHEO 3:12** “Naam, na wote wapendao kuishi maisha katika Yesu Kristo wataudhiwa”. Usifadhaishwe na dhiki yeyote itakayo tokana na kuokoka kwako. Hizo ni dhiki tumewekewa. **1WATHESALONIKE 3:3** “Mtu asifadhaishwe na dhiki hizik, maan anyingi enyewe mnajua ya kuwa twawekewa hizo”. Ni heri na thawabu kuu ukivumilia mateso yoyote kwaajili ya Yesu Kristo. Thawabu yako mbinguni ni kubwa mno unapovumilia. **1PETRO 3:14** “lakini mja poteswa kwaajili ya haki mna heri. Msiogope kutishwa kwao, wala msifadhaike; bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu:. Furahini kwa ajili ya hayo kwaajili ya Kristo Bwana. Maana ni afadhali kuteshwa kwa kutende mema, ikiwa ndiyo mapenzi ya Mungu kuliko kwa kutenda mabaya.

Baada tu yaw ewe kuokoka, Yesu Kristo amekaa pembeni na kukuangalia jinsi utakavyolitetea jina la Bwana wako kwa garama yoyote. Kama umepandwa kwenye udongo mzuri basi utavumilia dhiki kwaajili ya Kristo. Lakini kama umepandwa kwenye miamba, utakuwa umepokea wokovu kwa furaha lakin zikitukia dhiki au udhia kwaajili ya wokovu wako basi unachukizwa na kuacha wokovu. Ukifanya hivyo, utamhusuzinsha mna Bwana Yesu.

MATHAYO 13:20-21 “naye aliyepandwa kwenye miamba, huyu ndiye alisikiaye Neno, akalipokea mara kwa mara kwa furaha; lakini hana mizizi

ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au udhia kwaajili ya lile neno, mara huchukizwa.”

Ukipigwa makofi au fimbo kwasababu umetoka kanisani, ni heri kwako ujue thawabu yako ni kubwa mbinguni. Ukisingiziwa uongo kwaajili ya wokovu wako, thawabu yako ni kuu mno mbinguni utalipwa furaha kuul! **MATHAYO 5:11-12** “Heri nyi8nyi watakapo washutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwaajili yangu. Furahini na kushangilia kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mno mbinguni; kwaamana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.

Mbele za Mungu, ni sifa kubwa kupigwa makofi kwaajili ya wema. Kwaajili ya wokovu. Huu ndio wema hasa mbele za Mungu. Biblia inasema katika **1PETRO 2:19** “maana huu ndio wema hasa, mtu akivumilia huzuni, hasa kwa kumkumuka Mungu pale alipoteswa isivyo haki. Kwa maana ni sifa gani, kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili mtendapo mema na kupata mateso, huu ndio wema hasa mblee za Mungu. Kwasababu ndiyo mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwaajili yenu akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake”. Zifuate nyayo za Kristo. Dhiki yoyote itakuwa ni ya kitambo kidogo tu, lakini dhiki hiyo itakufaniia utukufu mwingi mno mbinguni; viangalie visivyoonekana kwanza.

2WAKORINTHO 4:17-18, “maana dhiki yenu nyepesi; iliyo ya muda wa kitambo kidogo tu, yatufanyia utukufu wa milele. **1PETRO 4:13-14** “lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini ili na katika ufunuo wa utukufu wake ufurahi kwa shangwe. Mkilaumiwa kwaajili ya jina la Kristo, ni heri yenu kwa kuwa Roho wa utukufu wa Mungu anawakalia **YAKOBO 5:10**. ndugu watwaeni manabii walionena kwa jina la Bwana, awe mfano wa kustahili mabaya na wa uvumilivu.

Wale mitume kumi na mmoja aliwaacha Yesu Kristo baada ya Yuda Israriote kujinyonga baada ya kumsaliti Yesu, wote kasoro mmoja walikufa vivyo vya kutisha kwaajili ya kuutetea wokovu. Hata hivyo hawakutetereka hadi mwisho. Kulingana na maandishi wa karne ya kwanza na ya pili, kuliko hao wane walisulubishwa kama Yesu Kristo. Petro alisulubishwa miguu juu kichwa chini huko roma. Andrea naye alisulubishwa katika nchi ya Misri na simon Mkananayo kama Paulo. Alikatwa huko roma kwa amri ya mfalme Nero. Ufalme wa Mungu unapatikana kwa njia ya dhiki nyingi. Ukisema kweli kazini utachukiwa na wote lakini shikilia uzi, liinue Jina la Yesu Kristo. Taji kubwa inakungojea.

JAMBO LA KUKUMBUKA

Watu wanaotutesa inabidi tuwaombe ili na wao waokoke. Tuwajibu kwa upole tu maana jawabu la upole hugeuza hasira hata hivyo tuzidi kumshika Yesu Kristo kwa gharama yoyote. **MITHALI 15:1** “Jawabu la upole hugeuza hasira;bali neno liumizalo huchochea ghadhabu.” Kumbuka tu kwamba katika wote tutakuwa pamoja; nia yetu ni moja, na tutasaidiana katika nyakati za kuteswa na kuudhiwa. Kiungo kimoja kinapoteseka kama ni kodole, basi mwili mzima uteseke. Ukitesea wewe basi kanisa zima litateswa. Jipe moyo utashinda.

KWAAJILI YA KRISTO

MATHAYO 10:37;-apendaye Baba au mama kuliko mimi hanistahili, wala apendaye mwana kuliko mimi hanistahili.

MATHAYO 10:29 Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba au mama au Watoto au mashamba, kwaajili ya Jina langu, atapokea mara mia, na kauurithi uzima wa milele.

MATHAYO 10:34 Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani, la! Siuja kuleta amani dunaini, bali upanga.

LUKA Je! Mwandani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani: nawambia, la sivyo, bali mafarakano.

MATHAYO 8:21 mwingine katika wanafunzi wake, akamwambia, Bwana nipe ruhusa niende nikamzike baba yang.

LUKA 9:59; akamwambia mwingine, nifuate. Akasema, bwana nipe ruhusa kwanza niende nikamzika baba yangu.

2WAKORINTHO 4:9 Twaudhiwa, bali hatuachwi, twatupwa chini bali hatuangamizwi.

1WAKORINTHO 15:30-31 Na sisi kwa nini tumo hatarini kila siku? Naam, ndugu, kwa huku kujisifu niliko nako juu yenu katika Kristo Yesu Bwana wetu ninakufa kila siku.

UFUNUO 2:10 usiogope mambo yatkayokupata, tazama huyo ibilisi atawatupa baadhi netu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, name nitakupa taji ya uzima.

YAKOBO 1:2-4, Heri mtu Yule astahimiliye majaribu, kwasababu akishakubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana livyowaadiki wampendao.

1WAKORINTHO 10:13 Jaribu halikuwapata ninyi isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ile Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu, atafanya na mlango wa kutokea ili muweze kustahimili.

WAEBRANIA 2:18 na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, anaweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.

YAKOBO 1:13-14. Mtu ajaribiwapo, asiseme ninajaribiwa na Mungu. Maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe kumjaribu mtu. Lakini kila mmoja hujaribiwa na shetani.

SOMO LA SABA

FURAHA KATIKA MAISHA YA WOKOVU

Mstari wa moyo **MITHALI 16:20B** “ Na kila amwaminiye Bwana ana heri”

Furaha ya wokovu

Ni vigumu kujifunza katika somo moja kwama hili furaha zinazoandamanan a wokovu. Hata hivyo, tutaangalia kwa ufupi sana maeneo machache katika furaha hii, maana furaha hii haina mwisho. Inaanzia hapa duniani na itaendelea mbinguni milele na milelel. Siku ile ulipokata hsairu na kuokoka, ulifanyika kuwa mtoto wa Mungu. Tunasoma katika **YOHANA 1:12-13**, bali wote waliompokwa aliwapa uwezo wa kufanyika kuwa Watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina lake, waliozaliwa si kwa damu wala si kwa mapenzi ya mwili, wala I kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu. Wewe sada ni mtoto wa Mungu. Hap mwanzo wewe ulikuwa mtoto wa ibilisi kwasababu kila atedaye dhambi ni wa ibilisi na tamaa zaibilisi ndizo apendazo kuzitenda. **YOHANA 8:44, 1YOHANA 3:7-8**. Sasa basi kwa kuwa wewe sasa ni mtoto wa Mungu, Mungu anajishughulisha mno na mambo yako yote. Kwa sababu hiyo mkono wa Mungu uko juu yako katika mambo yafuatayo;

a. ULINZI.

Kwa kuwa wewe umekuwa mtoto wa Mungu, ukamcha au kumhofu na kuisikia sauti yake alaipokuita na ukatubu dhambi zako, Mungu anakuangalia kwa namna ya ajabu maana ni mtoto wake. Mtegemee yeye tu, namna zozote za kutegemea hirizi kukulinda au kuogopa

wachawi nk. Hazina nafasi tena kwako. Unapoonewa sasa, Mungu ndiye anayekutetea moja kwa mja maana kila jambo kwako linamusu Mungu aliye baba yako. Huna haja ya kuogopa tena maandiko yafuatayo n I kwaajili yako. **ZEKARIA 2:9** “kwa maana Bwana wa majeshi asema hivi, ili nitafute utukufu amenituma kwa mataifa wale waliowateka ninyi; maana yeye awagusaye ninyi aigusa mboni ya jicho kake **ZABURI 34:7** malaika wa Bwana hufanya kituo akiwazungukia wamchao apate kuwaokoa.

2MAMBO YA NYAKATI 16:9 “kwa maana macho ya Bwana hukimbia kimbiba duniani mwote ili ajionyeshe mwene nguvu kwaajili ya hao, aliokamilika moyo kuelekea kwake. **ZABURI 91:4-7**, <wa manyoya yake atakufunika, chini ya mbawa zake utapata kimbilio; uaminifu wake ni ngao na kigao. Hutaogopa hofu ya usiku wala mshale urukao mchana, wala taufi ipitayo gizani, wala uele uharibuo adhuhuri, ijapokuwa watu elfu waanguka ubavuni mwako, naam, kumi elfu mkono wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe. **ZABURI 125:2** “kama milima inavyozunguka Yerusalemu, ndivyo Bwana anavyowazunguka watu wake, tangu ssa na hata milele. **KUMBUKUMBU LA TORATI 11:10-12**

b. WATU WANAOKUPIGA VITA/WANAOKUONEA

Kuanzia ulipokata shauri kuokolewa wewe ni mwa thamani mno machoni pa Mungu, hivyo vita si vyako tena bali vya Bwana wako YesuKristo **2MAMBO YA NYAKATI 20:15**. Yeye ni mtu wa vita **KUTOKA 15:3**, na ana uwezo wote wa kukupigania. Bwana atakupigania wewe, nawe utanyamaza kimya **KUTOKA 14:14. YAFUATAYO NI MAANDIKO YA Mungu kwaajili yako:-**

YEREMIA 15:20-21 “Nami nitakufanya kuwa kama ukuta wa bomba la shaba juu ya watu hawa, nao watapigana nawe lakini hawataushinda; maana mimi nipo pamoja nawe ili nikuokoe, na kukuponya, asema Bwana. Name nitakuokoa na mkono wa watu wabaya, name nitakukomboa katika mkono wao wenye kutisha.

ISAYA 54:17, “kila silaha itakayofanykia juu yako haitafanikiwa, na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa. huo ndio urithi wa watumishi wa Bwana na haki yao inayotoka kwangu mimi asema Bwana wa Mejeshi.

ISAYA 41:11-12, “ Tazama, wote walioona hasira juu yako watatahayarika na kufaidika; watu washindanao nawe watakuwa si kitu, na kuangamia. Utawatafuta wala hutawaona wale wapiganao nawe; watakuwa si kitu; watakuwa kama kitu kisichokuwa wale waliofanya vita juu yako.

ISAYA 43:4 “kwa kuwa ulikuwa wa thamani machoni pangu, na mwenye kuheshimiwa, name nimekupenda; kwa sababu hiyo nitatoa watu watu kwa ajili yako; na kabila za watu kwaajili ya maisha yako.

ISAYA 49:26, “ na hao wanaokuonea nitawalisha nyama yao wenyewe, nao wataelewa kwa kuinywa damu yao wenyewe, kama kwa mvinyo mpya; na wote wenyemwili watajua ya kuwa mimi, Bwana ni mwokozi wako, na mkombozi wako ni mwenye enzi wa Yakobo.

ISAYA 51:7-8, nisikilizeni, ninyi mjuao haki watu wambao mioyoni mweni mna sheria yangu; msiogope matukano ya watu, wala msifadhaike kwa sababu ya dhihaka zao. maana nondo itawala kama vazi, na funza atawala kama sufu; bali haki yangu itakuwa ya miele na wokovu wangu hata vizazi vyote.

ISAYA 43:1-2, “lakini sasa Bwana aliyekuhuluku, Eee Yakobo yeye aliyekuumba, Ee Israel, asema hivi, usiogope, maan animekukomboa, nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu. Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito haitakugharikisha, uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza.

c. MAGONJWA

Mapenzi yake Kristo aliyekuokoa ni kwamba uwe na uzima tena uwe nao tele.

YOHANA 10:10, Kazi za magonjwa ni za ibilisi na Yesu Kristo alidhihirishwa ili azivunje kazi za Ibilisi. **1YOHANA 3:8**. Litumie Jina la Yesu kukemea lolote linalokutesa wakati wowote na yaamini maandiki yafuatayo kwaaili ya uzima wkao. **ZABURI 34:19** “mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Bwana humponya nayo yote”.

KUTOKA 15:26, “ akamwambia, kwamba utaisikiliza kwa bidii sauti ya Bwana Mungu wako na kuyafanya aliyoelekezwa mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu

yako maradhi yoyote niliyowatia wamisri kwa kuwa mimi ndimi Bwana nikuponyaye.

YEREMIA 30:17 maana nitakurudishia afya, Nami nitakuponya jeraha zako, asema Bwana kwa sababu wamekuita mwenye kutupwa wakisema, ni sayuni ambao hapana mtu autakaye”

KUMBUKUMBU LA TORATI 7:15, “ na Bwana atakuondolea ugojwa wote; wala hatatia juu yako maradhi yoyote mabaya yujauyo ya misri.

d. MAOMBI

Maombi yako kabla ya kuokoka mbele za Mungu yalikuwa ni kama kelele tu. Mungu alikuwa hakusikilizi. Dhambi zilikutenganisha naye **ISAYA 59:2** “ Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia: baada yaw ewe kuokoka, Mungu anapenda mno kukusikia na kukutimizia haja zako. Katika kila hitaji lako sasa mtwike fadhaa zako zote Yesu Kristo katika maombi na utaona jinsi anavyokujibu maombi yako. Lolote lile ambalo ni mzigo kwako, mwombe Bwana naye atashughulika nalo. **ZABURI 55:22**, “umtwike Bwana mzigo wako naye atakugemeza, hatamwacha mwenye haki aondoshe milele. Soma pia **1PETRO 5:7, YOHANA 16:24**, “hata sasa hamkuomba neno kwa Jina langu;ombeni, nanyi mtapata furaha yenu iwe timilifu.

1YOHANA 5:14-15, Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atatusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba. Katika maombi kumbuka jambo moja;mwombe Mungu kwa Jina la Yesu Kristo siyo kupitia kwa mtakatifu petro, Paulo, andrea au bikira maria. Hivyo siyo sahihi. **YOHANA 14:13-14**, “nanyi mkiomba lolote kwa Jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani yaMwana. Mkinomba Neno lolote kwa jina langu, nitalifanya. Bikira maria naye alimwomba Yesu **MATENDO 1:14**. Hatupaswi kumwomba Mungu kupitia kwa maria au mtu yeyote maana kufanya hivyo ni kufanya mtu huyo achukue nafasi ya Yesu Kristo. Huko ni kulitia unajisi Jina la Bwana **ISAYA 48:11**. Jina la Yesu ni Jina lililo juu ya majina yote. **WAFILIP 2:9-10**. “kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno akamkirimia Jina lile lipitalo kila Jina; ili katika Jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi”. Kama nilivyosema ni vigumu kuzitaja furaha zote zinazokukaa ili katika

maisha ya wokovu katika somo moja kwasababu wewe ni kiumbe kipya na furaha mpya nyingi zinaandamana nawe. Yote ni mapya **2WAKORINTHO 5:17** “hata imekuwa amtua akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama yamekuwa mapya. “ lakini somo litakuwa halijakamilika ikiwa sitakuambia furaha nyingine katika furaha hizo nyingi mpya.

e. KUANZIA SASA UNA NDUGU WENGI USIO WAJUA.

Ulipokata shauri kuokolewa, umeingia katika familia ya Mungu inayoongowa na mzaliwa wa kwanza Yesu Kristo. Wote tuliomo katika familia hii ni ndugu. Mimi siyo ndugu yko kimwili, lakini sasa ni zaidi ya ndugu yako kimwili. Vivyo hivyo kila ndugu aliye katika Kristo ni ndugu yako awe yuko katika nchi hii au popote duniani. Hakuna mipaka ya nchi, wala kabila, lugha au rangi. Kila mmoja nitajishughulisha naye. Mimi tangu niingine katika familia hii sijaona upendo wa ajabu kama niliouona katika familia hii. Ndugu wa kimwili watakupinga lakini kwa ndugu wa kiroho utapata faraja tele. Karibu katika familia ya ndugu wengi. **WARUMI 8:29**. “ maan awale waliowajua tangu asili, aliwahugu tangu asili, wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

SOMO LA NANE

Jinsi ya Kuukulia Wokovu

Mustari wa moyo **1PETRO 2:2** “kama Watoto wachanga waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.”

Kuukulia wokovu

Biblia inasema katika **YOHANA 3:6**, “kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, na kilichozaliwa kwa Roho ni rorho. Wewe sasa baada ya kutubu dhambi zako na kusamehewa, umezaliwa kwa roho, ndiyo maana inatajwa pia kwamba umezaliwa mara ya pili. Hapo mwanzo ulizaliwa katika mwili, na kilichozaliwa kwa mwiili hakiwezi kuishinda dhambi. Sasa umezaliwa mara ya pili na ufalme wa Mungu ni wako. Sasa basi, tunapenda tuangalie jambo moja la muhimu sana. Mtoto mchanga anapokuwa amezaliwa kwa mwili yaani katika hali yakawaida ya inadamu; ili aendelee kuish ni lazime apewe maziwa au siyo akiahcwa tu hiyo atakufa. Vivyo hivyo na kilichozaliwa kwa aRoho. Hiki nacho

kinahitaji maziwa au siyo kitakufa hakika. Mtu baada ya kuzaliwa mara ya pili, ni lazim atamani maziwa ili aweze kukua, au siyo atadumaa na hatimaye kufa kiroho na kurudi kumtumikia shetani. Ili mtu aliyezaliwa mara ya pili aendele katika wokovu ni lazima anywe maziwa ya kiroho. **1WAKORINTHO 3:1-2**, “kama na Watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa..**WAEBRANIA 5:13**, “kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hauwi sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Baada tu yakuzaliwa mara yapili au kuokolewa, tunakuwa bado hatujui sana neno la haki; tunahitaji maziwa ili tuweze kukua katika wokovu.

MAZIWA HAYA NI NINI?

Maziwa haya ni kinywaji cha roho kinachotoka kwa Yesu Kristo ambacho ni Neno la Kristo, kama tunavyosoma katika **1KORINTHO 10:4** “***Wote wakanywa kinywaji kile cha roho; kwa maana waliunywea mwamba wa roho uliowafuata:***

Na mwamba ule ulikuwa ni Kristo. “Bila kupata mafundisho ya Neno la Mungu, mtu yeyote aliyezaliwa mara ya pili lazima atadumaa na hatimaye kufa kiroho na kurudi tena katika utumwa wa dhambi. Hakuna uwezekano wowote wa mtu kuendelea katika wokovu bila kupata mafundisho ya Neno la Mungu. Hili ni kwasababu Neno la Mungu lina sehemu kubwa mno katika maisha ya kiroho ya mtu. Neno la Mungu lina faida zipi katika maisha ya kiroho ya mtu aliyeokoka?

1) NENO LA MUNGU NI CHAKULA CHA KIROHO

Mtu aliyeokoka hawezi kuishi kwa mkate tu wa kawaida. Mkate wa kawaida unaukuza na kuupa nguvu mwili tu. Mtu wa rohoni yeye naye ni lazima apate Neno la Mungu ili apate furaha na shangwe ya moyo wake.

Tunasoma kaitika **YEREMIA 15:16**, “***Maneno yako yalionekana, name niliyala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu; maana nimeitwa kwa jina lako, wewe Bwana Mungu wa majeshi. Maneno ya Mungu ni chakula halisi chenye uwezo wa kumkuza mtu kiroho na kumhakikishia uzima wa milele.***

Tukitaka kuishi milele ni lazime tumle Yesu. Kumla Yesu ni lulila Neno la Mungu maana Yesu ni Neno la Mungu. **YOHANA 1:1, UFUNUO 19:13, YOHANA 6:48-58**. Tukiacha kulila Neno la Mungu baada ya kuzaliwa mara ya pili, hatuwezi kuishi milele. Chakula cha kawaida hata kiwe kizuri kama mana

bado kitamfanya mtu afe na kuukosa uzima wa milele. Baada ya kuokolewa hatuna budi kukipa uzito mkubwa chakula cha kiroho yaani Neno la Mungu, ili tuishi milele na Yesu Kristo mbinguni. Tunasoma katika **YOHANA 6:48-49, 57-58, *Mimi ndimi chakula cha uzima. Baba zentu waliila mana jangwani; wakafa. Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, name ni hai kwa Baba;kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi.hiki ndicho chakula kishukacho kutoka mbinguni; si kama mababa walivyokula wakafa, bali akilaye chakula hicho ataishi milele.***

Tena tunasoma ktika **MATHAYO 4:4**, na pia katika **KUMBUKUMBU 8:3**, “Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiyojua wewe wala baba zako hawakujua, apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana. Kwa namna yoyote ile, hata kama mtu alipozaliwa mara ya pili alipata badiliko kubwa namna gani; kukua kwake kiroho kunategemeana na chakula anachokula cha kiroho. Au siyo atakufa kiroho, hataendelea na wokovu. Mungu anakupenda mno kaka au dada, ndiyo maana anakufundisha leo kuwa inakubidi upende mafundisho leo kuwa inakubidi upende mafundisho ya Neno la Mungu kuliko hata chakula cha mwili. Watu wa Mungu waliokuwa juu sana kiroho, wote walikuwa na tabia hiyo ya kupenda sana kusikia na kusoma Neno la Mungu hivyo Mungu anakuwepo kwa wingi ndani yake, kwasababu Neno la Mungu lina nguvu ile ile ya Mungu, na ndiye Mungu mwenyewe.

AYUBU 23:12, *sikurudi nyuma kuiacha amri ya midomo yake; nimeyatunza maneno ya kinywa chake (Mungu) zaidi ya riziki yangu.*
ZABURI 119:72, *Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu, kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.*

2) NENO LA MUNGU NI TAA NA MWANGA WA NJIA YETU YA MBINGUNI

Njia ya mbinguni ni nyembamba sana, kwa maneno mengine imesonga mno; na mlango wa mbinguni ni mwembamba sana **MATHAYO 7:13**. Inabidi wakati wote tuwe na taa na mwanga unaotumulikia mbele tuendako. Inafananishwa na mtu anayetembea wakati wa usiku juu ya daraja jembamba lililojengwa juu ya bahari. Bila mtu huyo kuwa na taa na mwanga, ni rahisi sana kuangukia baharini. Ulimwengu huu ni bahari, ni njia pana. Yesu alituokoa, ametuokoa kutoka katika bahari hiyo na kutuweka juu ya daraja jembamba. Kufika kwetu tunakokwenda, kunategemea sana jinsi ambavyo tutaling’ang’ania Neno la Mungu ambalo ndilo taa na mwanga wa njia hii. Tukiliacha Neno la Mungu ni dhahiri kabisa kwamba tutapoteza wokovu wetu na kuangukia tena bahari au

katika njia pana. Neno la Mungu linasema katika **ZABURI 119:105**, “*Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu.*”

Tunasoma pia katika **MITHALI 6:21-23**, “*Yafunge hayo katika moyo wkao daima; jivike hayo shingoni mwako. Uendapo yatakuongoza, ulalapo yatakulinda, na uamkapo yatazungumza nawe. Maana maagizo hayo (ya Mungu) ni taa, na sheria hiyo ni nuru.*”

3) NENO LA MUNGU NI SILAHA YA USHINDI JUU YA DHAMBI

Ni vigumu kabisa kuishinda dhambi bila Neno la Mungu. Yesu Kristo katika **MATHAYO 4**, alimshinda shetani alipokuja kumjaribu, kwa kulitumia Neno la Mungu alipokuwa akisema “imeandikwa”. Huwezi kuishinda dhambi au majaribu ya shetani ikiwa hupendi mafundisho ya Neno la Mungu. Shetani atakushinda tu. Dhambi itakushinda. Dhambi inawezwa na kushindwa kwa Neno la Mungu pekee. Biblia inasema katika **ZABURI 119:11** “*Moyoni mwangu nimeliweka Neno lako, nisije nikakutenda dhambi*”.

Kadiri tunavyoisafisha njia yetu na kuifanya safi (ZABURI 199:9) yaani kwa kulitenda Neno lake, kwa maana nyingine ni kwamba maisha yetu ya kiroho yanafanywa safi kwa Neno la Mungu YOHANA 15:3. Tukiacha kuyapenda na kuyafuata mafundisho ya Neno la Mungu, tunaweza tukafanya dhambi pasipo kujua ni dhambi, na hilo bado linatufanya tuwe na hatia mbele za Mungu. Neno la Mungu linasema katika MAMBO YA WALAWI 15:17, na kama mtu akifanya dhambi, na kutenda mambo hayo mojawapo ambayo Bwana alizuilia yasifanywe, ajapokuwa hakuyajua, ni mwenye hatia vivyo, naye atachukua uovu wake. Kwa sababu hii, inatubidi tuwe tayari wakati wote kuyatafuta mafundisho ya Neno la Mungu, ili tusimtende Bwana wetu dhambi. Ni wajibu wetu sisi kujifunza Neno la Mungu, ili tujue nini ni dhambi na nini si dhambi, na ili tuiepuke dhambi, kwasababu kama tukifanya mambo ya dhambi bila kujua kwetu, bado ni dhambi tu mbele za Mungu, Mungu hatasema hatujatenda dhambi kwasababu ati hatukujua. Hivyo utakuta ni muhimu sana kujifunza Neno la Mungu na kulifuata kama lilivyo.

YESU ANARUDI, TUJIANDAE!